

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 63 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** MEI 2026

KAMATI YA BUNGE YARIDHISHWA NA UBORA WA UJENZI OFISI ZA TSC, YATAKA KASI IONGEZWE



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI wakikagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika eneo la Njedengwa, Dodoma, tarehe 3 Mei, 2026.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

Walimu: Nguzo Imara ya Maendeleo ya Taifa

Katika kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani, Mei Mosi 2026, Serikali inatoa pongezi za dhati kwa walimu wote nchini kwa mchango wao mkubwa katika kukuza elimu na maendeleo ya Taifa. Walimu wameendelea kuwa nguzo muhimu katika kujenga rasilimali watu yenye maarifa, ujuzi na maadili mema, hali inayochangia moja kwa moja ustawi wa jamii na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Katika kipindi hiki cha mabadiliko ya sayansi na teknolojia, walimu wameendelea kuonesha weledi na ubunifu katika kufundisha na kulea wanafunzi ili waendane na mahitaji ya dunia ya sasa. Pamoja na changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza katika mazingira ya kazi, walimu wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu, uvumilivu na kujituma, jambo linalostahili kutambuliwa na kuthaminiwa.


Serikali kwa upande wake imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha sekta ya elimu, ikiwa ni pamoja na kuimarisha

miundombinu ya shule, kuongeza upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, pamoja na kuboresha maslahi ya walimu kadri uwezo unavyoruhusu. Juhudi hizi zinalenga kuhakikisha kuwa walimu wanafanya kazi katika mazingira bora zaidi yatakayowawezesha kutoa elimu yenye ubora unaokusudiwa.

Aidha, walimu wanahimizwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii, kuzingatia maadili ya taaluma yao, na kutumia mbinu bunifu katika ufundishaji ili kuongeza ufanisi wa ujifunzaji kwa wanafunzi. Walimu wanapaswa kuendelea kujifunza na kutumia teknolojia kwa usahihi ili waweze kukidhi mahitaji ya elimu katika karne ya sasa.

Kwa pamoja, tuendeleo kuthamini na kuenzi mchango wa walimu katika Taifa letu. Maadhimisho ya Mei Mosi ya mwaka huu yawe chachu ya kuimarisha mshikamano, uwajibikaji na ari ya kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya Taifa na vizazi vijavyo.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina M. Nkwama

Wajumbe
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera
Apsa Othman
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu
Artemony T. Vincent

Mhariri
Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 756 927 131 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

KAMATI YA BUNGE YARIDHISHWA NA UBORA WA UJENZI OFISI ZA TSC, YATAKA KASI IONGEZWE

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeridhishwa na ubora wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) unaoendelea katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma, huku ikimtaka mkandarasi, SUMA JKT kuongeza kasi ya kukamilisha mradi.

Akizungumza baada ya kukagua mradi huo tarehe 03 Mei, 2026, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Florent Kyombo, alisema pamoja na kazi iliyofanyika kufikia viwango vinavyokubalika, bado kuna haja ya kuongeza kasi ya utekelezaji ili kuhakikisha watumishi wa TSC wanapata mazingira bora ya kufanya kazi kwa wakati.

Alibainisha kuwa Serikali imewekeza takribani shilingi bilioni 6.4 katika mradi huo, hivyo matarajio ni kuona thamani ya fedha inaakisiwa kupitia ubora, weledi na ukamilishaji kwa wakati.

Kamati hiyo pia iliagiza uongozi wa TAMISEMI kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi wa Walimu kupitia upya baadhi ya vipengele vya mkataba ili kuwezesha mkandarasi kupata mazingira wezeshi ya kukamilisha kazi kwa wakati.

Aidha, Mhe. Kyombo alisema Kamati itashauri Serikali kufanya maboresho ya kisheria yatakayoweza kampuni ya SUMA



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI wakikagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika eneo la Njedengwa, Dodoma, tarehe 3 Mei, 2026.

JKT kupata mikopo kutoka taasisi za fedha, sawa na kampuni nyingine za ujenzi ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya umma.

Awali, akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya mradi Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama, ilielezwa kuwa mradi huo unatekelezwa kwa utaratibu wa Design and Build, ambapo mshauri na mtekelezaji mkuu ni SUMA JKT kupitia kampuni zake za ushauri na ujenzi.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hadi tarehe 3 Mei, 2026 ujenzi umefikia asilimia 71 huku mkandarasi akiwa amelipwa shilingi bilioni 2.6, sawa na asilimia 40 ya thamani ya mkataba.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa hatua zilizobaki ni za umaliziaji ambazo zinahitaji gharama kubwa kwa

wakati mmoja, ikiwemo ununuzi wa vifaa kama lifti, vigae na mifumo ya viyoyozi.

Kwa upande wake, mwakilishi wa mkandarasi kutoka SUMA JKT Kanda ya Kati, Meja Samweli Jambo, alisema fedha zilizopokelewa hadi tarehe 30 Aprili, 2026 zinaendana na kazi iliyotekelezwa, huku akisisitiza umuhimu wa upatikanaji wa fedha kwa wakati ili kukamilisha mradi huo bila kuchelewa.

Naye Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mhe. Jaffar Salum Seif alisema Serikali itafanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na Kamati hiyo, ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati madhubuti itakayoiwezesha SUMA JKT kukamilisha mradi huo kwa wakati.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI wakisikiliza maelezo ya maendeleo ya mradi kutoka kwa mkandarasi, SUMA JKT, wakati wa ziara ya ukaguzi wa mradi huo tarehe 3 Mei, 2026 katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI wakitoa maelekezo kwa mkandarasi SUMA JKT kuongeza kasi ya ujenzi ili mradi ukamilike kwa wakati.

KAMATI YA BUNGE YARIDHISHWA NA UBORA WA UJENZI OFISI ZA TSC, YATAKA KASI IONGEZWE



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI, Mhe. Florent Kyombo, akiiongoza kikao cha tathmini ya mradi wa ujenzi wa ofisi za TSC wakati wa ziara ya Kamati hiyo Njedengwa, Dodoma tarehe 3 Mei, 2026.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mhe. Jaffar Salum Seif, akitoa neno la shukrani kwa Kamati ya Bunge baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa ofisi za TSC Njedengwa, Dodoma.



Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke, akizungumza wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI kwenye mradi wa ujenzi wa ofisi za TSC Njedengwa, Dodoma.

Naibu Katibu Mkuu (Elimu), Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, ndugu Atupele W. Mwambene, akitoa maelezo wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI Njedengwa jijini Dodoma.

KAMATI YA BUNGE YARIDHISHWA NA UBORA WA UJENZI OFISI ZA TSC, YATAKA KASI IONGEZWE



Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi za TSC mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI tarehe 3 Mei, 2026 katika eneo la mradi Njedengwa jijini Dodoma.



Muonekano wa jengo la ofisi za TSC linaloendelea kujengwa Njedengwa, Dodoma likiwa katika hatua za mwisho huku jitihada zikielekezwa kukamilisha mradi kwa wakati.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI Akagua Ujenzi wa Ofisi za TSC Dodoma, Aagiza Kuongezwa Kasi ya Utekelezaji

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Miundombinu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhandisi Rogatus H. Mativila, tarehe 23 Aprili, 2026 ametembelea na kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) unaoendelea katika eneo la Njedengwa, jijini Dodoma.

Ziara hiyo imelenga kufuatilia utekelezaji wa mradi huo muhimu wa Tume unaotarajiwa kuboresha mazingira ya kazi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu nchini.

Katika ukaguzi huo, imeelezwa kuwa ujenzi wa jengo hilo umefikia asilimia 74 ya utekelezaji. Kufuatia hatua hiyo, Mhandisi Mativila amemtaka Mkandarasi SUMAJKT kuandaa mkakati wa kina na mpangokazi madhubuti utakaowezesha kuongeza kasi ya ujenzi, ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa haraka.

Amesisitiza kuwa pamoja na kuongeza kasi ya utekelezaji, ni muhimu kuzingatia viwango vya ubora vinavyotakiwa katika ujenzi wa miradi ya umma ili kuhakikisha jengo hilo linadumu kwa muda mrefu na kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa.

Kwa upande wake, Mkandarasi SUMAJKT ameahidi kuimarisha utekelezaji wa mradi huo kwa kuongeza rasilimali na nguvu kazi, akieleza kuwa hatua zaidi zitachukuliwa kuhakikisha ujenzi unakamilika kwa wakati uliopangwa.

Kabla ya kufika katika eneo la mradi, Mhandisi Mativila alikutana na Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu, ambapo alipata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume pamoja na maendeleo ya mradi huo.

Katika kikao hicho, ameipongeza Tume kwa juhudi inazozifanya katika kutoa huduma kwa walimu nchini na kusisitiza umuhimu wa kuendelea kuboresha mifumo ya kiutendaji ili kuimarisha zaidi sekta ya elimu.

Aidha, ameeleza kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itaendelea



Naibu Katibu Mkuu (Miundombinu) kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Mhandisi Rogatus H. Mativila, akitoa maelekezo wakati wa ziara yake ya kukagua mradi wa ujenzi wa Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu unaoendelea katika eneo la Njedengwa, Dodoma tarehe 23 Aprili, 2026.

kushirikiana kwa karibu na Tume ili kuhakikisha mazingira bora ya kazi yanakuwepo na kuchochea utekelezaji mzuri wa majukumu yake.

Akitoa ufafanuzi kuhusu maendeleo ya mradi huo, Katibu

wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwalimu Paulina Nkwama, amesema mradi huo ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Tume ili kutoa huduma bora kwa walimu nchini.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI Akagua Ujenzi wa Ofisi za TSC Dodoma, Aagiza Kuongezwa Kasi ya Utekelezaji



Naibu Katibu Mkuu (Muundombinu) kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Mhandisi Rogatus H. Mativila (katikati), akirwa katika ukaguzi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu katika eneo la Njedengwa, Dodoma tarehe 23 Aprili, 2026. Upande wa kushoto ni Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (kulia), akitoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi za TSC kwa Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI tarehe 23 Aprili, 2026 jijini Dodoma.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI Akagua Ujenzi wa Ofisi za TSC Dodoma, Aagiza Kuongezwa Kasi ya Utekelezaji



Baadhi ya watumishi wa Tume wakiwa katika kikao na Naibu Katibu Mkuu (Miundombinu) kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI Mhandisi Rogatus H. Mativila (hayupo pichani) tarehe 23 Aprili jijini Dodoma.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI Akagua Ujenzi wa Ofisi za TSC Dodoma, Aagiza Kuongezwa Kasi ya Utekelezaji



Baadhi ya washiriki kutoka TSC na SUMA JKT wakiwa katika kikao na Naibu Katibu Mkuu (Miundombinu) kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI Mhandisi Rogatus H. Mativila (hayupo pichani) tarehe 23 Aprili jijini Dodoma.



Sehemu ya muonekano wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) unaoendelea kujengwa Njedengwa, Dodoma, ukiwa katika hatua za mwisho za utekelezaji.”



OFISI YA WAZIRI MKUU
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

MFANYAKAZI HODARI 2026



Paulino Brayson Kalinga

AFISA KUMBUKUMBU

*"Hongera kwa Juhudi, Bidii na Uweledi
katika Utendaji kazi Wako"*



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu



OFISI YA WAZIRI MKUU
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

MEI 1, 2026

MEI MOSI

HERI YA SIKU YA WAFANYAKAZI

**"Kazi zenye Staha ni Nguzo Imara kwa Maendeleo
Endelevu katika Utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050"**



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

TSC YAUNGANA NA WATUMISHI KUADHIMISHA MEI MOSI



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakipita mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule (hayupo pichani) wakati wa maandamano ya maadhimisho ya Mei Mosi 2026 yaliyofanyika kimkoa katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeungana na taasisi mbalimbali kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani, Mei Mosi, iliyofanyika tarehe 1 Mei 2026 katika maeneo mbalimbali nchini.

Kitaifa, maadhimisho hayo yamefanyika mkoani Njombe yakiongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Sambamba na maadhimisho hayo ya kitaifa, Mkoa wa Dodoma uliadhimisha siku hiyo kwa maandamano ya watumishi yaliyoanzia viwanja vya Bunge hadi uwanja wa Jamhuri.

Maandamano hayo yalikusisha makundi mbalimbali ya wafanyakazi kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali.

Mgeni rasmi katika maadhimisho ya ngazi ya mkoa alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, ambaye alipokea maandamano na kuzungumza na watumishi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Senyamule alisisitiza wafanyakazi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, nidhamu na weledi, akibainisha kuwa Serikali imefanya jitihada mbalimbali kuboresha maslahi ya wafanyakazi nchini.

Akifafanua zaidi, alisema changamoto za wafanyakazi zimepungua kwa kiasi kikubwa

kutokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali, huku akiahidi kuwa juhudi za kutatua changamoto zilizobaki zitaendelea kufanyika kadiri ya uwezo uliopo.

Kaulimbiu ya mwaka huu isemayo, "Kazi zenye staha ni nguzo imara kwa maendeleo endelevu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050," imeweka msisitizo katika umuhimu wa mazingira bora ya kazi, heshima kwa mfanyakazi na uwajibikaji kama msingi wa kufikia malengo ya muda mrefu ya maendeleo ya Taifa.

Ushiriki wa TSC katika maadhimisho hayo umeakisi dhamira yake ya kuendelea kusimamia ustawi wa walimu na kuimarisha utendaji kazi wao kwa manufaa ya sekta ya elimu na Taifa kwa ujumla.



Sehemu ya wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kufika uwanja wa Jamhuri Dodoma wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani tarehe 1 Mei, 2026.

TSC YAUNGANA NA WATUMISHI KUADHIMISHA MEI MOSI



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakishiriki maandamano kuelekea uwanja wa Jamhuri mkoani Dodoma wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kwa mwaka 2026 tarehe 1 Mei, 2026.

WALIMU MAKETE WAPONGEZA SERIKALI KWA KUIMARISHA MASLAHI NA MAZINGIRA YA KAZI

Na Mwandishi Wetu – Makete

Baadhi ya walimu wilayani Makete wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa kuboresha maslahi yao na mazingira ya kazi, hatua ambazo zimeongeza ari na ufanisi katika utoaji wa elimu.

Pongezi hizo zimetolewa wakati wa mahojiano na Maafisa wa Mawasiliano kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), yaliyolenga kuangazia mafanikio ya Serikali katika kuwahudumia walimu.

Mkuu wa Shule ya Msingi Ndulambo, Mwl. Raphael Jeremia Kalongola, alisema Serikali imefanikiwa kutatua changamoto

ya ucheleweshwaji wa upandishaji madaraja kwa walimu, hali iliyorejesha usawa na kuondoa malalamiko ya muda mrefu miongoni mwao.

“Hatua hii imeongeza morali ya kazi na kuondoa kinyongo kilichokuwepo kwa baadhi ya walimu waliokuwa wamebaki nyuma kimaslahi,” alisema.

Aliongeza kuwa Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga madarasa, nyumba za walimu, mabweni na vyoo, hatua iliyochangia kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Kwa upande wa teknolojia, alisema matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yamerahisisha utekelezaji wa majukumu ya walimu na kuishauri Serikali kuendelea kuimarisha upatikanaji wa mtandao katika shule zote ili kuongeza ufanisi zaidi.

Akizungumzia mitaala iliyoboreshwa, Mwl. Kalongola alisema ina mchango mkubwa katika kuandaa wanafunzi kuwa na ujuzi unaowawezesha kujiajiri na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Taifa.

Naye Mwalimu kutoka Shule ya Msingi Makete, Mwl. Upendo Jumanne, aliipongeza TSC kwa kuendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu kuzingatia Sheria, Kanuni

na Taratibu za utumishi, jambo linalosaidia kupunguza makosa ya kinidhamu.

Alisema kupitia mafunzo hayo, walimu wamepatiwa miongozo mbalimbali inayowawezesha kuelewa haki na wajibu wao pamoja na namna bora ya kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa taratibu za kazi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari Iwawa, Mwl. Fadhihi Eliezer, alisema Serikali imeboresha utendaji kazi wa watumishi wa umma kwa kulipa stahiki kwa wakati, ikiwemo fedha za likizo na upandishaji vyeo.

Alisema hatua hiyo imepunguza manung'uniko na kuongeza uwajibikaji kwa walimu ambao hapo



*Mkuu wa Shule ya Msingi Ndulambo,
Mwl. Raphael Jeremia Kalongola.*

*Mwalimu wa Shule ya Msingi Makete,
Mwl. Upendo Jumanne.*

*Mkuu wa Shule ya Sekondari Iwawa,
Mwl. Fadhihi Eliezer.*

awali walikaa muda mrefu katika daraja moja bila kupanda.

Aidha, alieleza kuwa utoaji wa ruzuku kwa shule pamoja na matumizi ya mifumo ya kidijitali kama TSCMIS umeongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu za walimu.

Kwa ujumla, walimu hao wameeleza kuwa hatua zinazochukuliwa na Serikali zimechangia kuimarisha sekta ya elimu kwa kuongeza motisha, uwajibikaji na ubora wa utoaji wa elimu.

BW. PAULINO KALINGA ANG'ARA MEI MOSI, AIBUKA MFANYAKAZI HODARI TSC 2026

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Afisa Kumbukumbu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulino Kalinga, ameibuka Mfanyakazi Hodari wa mwaka 2026 ambapo ametambuliwa katika maadhimisho ya Mei Mosi yaliyofanyika mkoani Dodoma.

Kalinga alikabidhiwa cheti na zawadi na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ikiwa ni sehemu ya utambuzi kwa wafanyakazi waliofanya vizuri kutoka taasisi mbalimbali wakati wa kilele cha maadhimisho hayo.

Akizungumza mara baada ya kupokea pongezi kutoka kwa watumishi wenzake, Kalinga alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema, nguvu na afya njema, huku akitoa shukrani zake kwa uongozi wa TSC kwa kumlea katika misingi bora ya kazi na kumwamini miongoni mwa watumishi wengi.

Alisema mafanikio hayo si yake binafsi bali ni matokeo ya ushirikiano wa wafanyakazi wenzake, akibainisha kuwa mshikamano wa timu ndiyo uliomuwezesha kufikia hatua hiyo.

“Nawashukuru sana wafanyakazi wenzangu kwa ushirikiano wao. Haya ni mafanikio ya pamoja, si yangu peke yangu,” alisema Kalinga.

Aliahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi na kujituma, sambamba na kuimarisha ushirikiano kazini ili kuongeza tija katika utendaji wa taasisi.

Katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisisitiza umuhimu wa kuthamini wafanyakazi bora, akieleza kuwa utambuzi huo ni chachu ya kuongeza ari ya kazi na ushindani chanya miongoni mwa watumishi.

Alibainisha kuwa Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kazi na kushughulikia changamoto za wafanyakazi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.



Afisa Kumbukumbu, Paulino Kalinga wa Tume ya Utumishi wa Walimu akipokea cheti cha Mfanyakazi Hodari wa TSC 2026 kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kwa ngazi ya mkoa yaliyofanyika tarehe 1 Mei, 2026 mjini Dodoma.



Afisa Kumbukumbu, Paulino Kalinga (wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Msaidizi Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mectilids Kapinga (wa kwanza kulia), Mkurugenzi Msaidizi Utawala, Apsa Othman (wa pili kutoka kushoto) na Mkurugenzi Msaidizi Nidhamu na Maendeleo ya Walimu, Asha Lubuva wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kwa ngazi ya mkoa yaliyofanyika tarehe 1 Mei, 2026 mjini Dodoma ambapo Bw. Kalinga akipokea cheti cha Mfanyakazi Hodari wa TSC kwa mwaka 2026.



Mfanyakazi Hodari wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa mwaka 2026, Paulino Kalinga (wa tatu kutoka kulia) akiwa pamoja na watumishi wa TSC wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kwa ngazi ya mkoa yaliyofanyika tarehe 1 Mei, 2026 mjini Dodoma.

TSC YAJENGEA UWEZO KAMATI YA UKAGUZI NA MENEJIMENTI KUIMARISHA UWAJIBIKAJI

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendesha mafunzo ya siku tatu kwa wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi, Menejimenti na Sekretarieti kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za umma na utekelezaji wa majukumu ya taasisi.

Akifungua mafunzo hayo kwa niabaya Katibu wa Tume, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Bw. Zachary Dida, alisema hatua hiyo inalenga kujenga uelewa wa pamoja kuhusu misingi ya ukaguzi wa ndani, usimamizi wa vihatarishi na uendeshaji wa taasisi kwa kuzingatia kanuni za utawala bora.

Alifafanua kuwa mafunzo hayo yamejikita katika kuimarisha uwezo wa Kamati ya Ukaguzi katika maeneo ya ukaguzi wa ndani unaozingatia viwango vya kimataifa, kanuni za fedha za umma pamoja na majukumu na wajibu wa kamati hiyo katika taasisi za umma.

"Tunatarajia mafunzo haya yataongeza uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma, pamoja na kusaidia kubaini na kushughulikia mapungufu katika mifumo ya kifedha," alisema Bw. Dida.



Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Bw. Zachary Dida, akifungua mafunzo hayo.

Aliongeza kuwa ujuzi utakaopatikana utaiwezesha kamati pamoja na menejimenti kuongeza thamani katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku na kuimarisha utawala bora ndani ya Tume.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, CPA Upendo Werema, aliipongeza menejimenti ya TSC kwa kuandaa mafunzo hayo, akibainisha kuwa yatawasaidia wajumbe kutekeleza wajibu wao

wa kutoa ushauri kwa Afisa Masuuli katika maeneo ya usimamizi wa vihatarishi, mifumo ya udhibiti na uendeshaji wa taasisi.

Alisema uelewa mpana wa masuala ya fedha, rasilimaliwatu na manunuzi ni muhimu kwa Kamati ya Ukaguzi ili kuhakikisha taasisi inafanya kazi kwa ufanisi na kuendelea kupata hati zinazoridhisha za ukaguzi.

Akiwasilisha mada katika mafunzo hayo, Mkaguzi Mkuu wa Ndani kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, CPA Alphonse Muro, alisema ushirikishwaji wa menejimenti, Kamati ya Ukaguzi na sekretarieti ni muhimu katika kuimarisha uelewa wa michakato ya kazi za taasisi na kuongeza ufanisi wa utendaji.

Alibainisha kuwa Kamati ya Ukaguzi ikiwa na uwezo wa kutosha itaweza kutoa ushauri unaoisaidia taasisi kuboresha huduma kwa wananchi na kuimarisha uwajibikaji.

Kwa ujumla, mafunzo hayo yanatarajiwa kuwa chachu ya kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani, kuongeza uwazi na kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi na kwa malengo yaliyokusudiwa.



Washiriki wa mafunzo ya kujengewa uwezo Kamati ya Ukaguzi, Menejimenti na Sekretarieti ya TSC wakiwa katika ufunguzi wa mafunzo.

TSC YAJENGEA UWEZO KAMATI YA UKAGUZI NA MENEJIMENTI KUIMARISHA UWAJIBIKAJI



Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, CPA Upendo Werema, akitoa maelezo ya utangulizi.



Mkaguzi Mkuu wa Ndani, CPA Alphonse Muro, akiwasilisha mada.

ELIMU YA UTUMISHI KWA WALIMU YAPUNGUZA MASHAURI YA KINIDHAMU NJOMBE

Na Mwandishi Wetu – Njombe

Utoaji wa elimu kwa walimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi umeanza kuzaa matokeo chanya katika Wilaya ya Njombe, ambapo idadi ya mashauri ya kinidhamu imeendelea kupungua kwa kasi kuanzia mwaka 2021.

Akizungumza katika mahojiano maalum, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Njombe, Bw. Msigala Philipo Kilasi, alisema mashauri hayo yamepungua kutoka nane (8) mwaka 2021 hadi matatu (3) mwaka 2026 katika halmashauri zote tatu za wilaya hiyo.

Alifafanua kuwa mafanikio hayo yanatokana na juhudi za makusudi za Tume kutoa elimu na ushauri wa kitaalamu kwa walimu kuhusu kuzingatia Sheria Kanuni na Taratibu za kazi, sambamba na kusambaza vitabu vya maadili na miongozo mbalimbali kwa walimu na viongozi wa shule.

“Tumekuwa tukitoa semina elekezi kwa walimu wapya, kusambaza nakala laini za miongozo ya maadili, pamoja na kutoa ushauri nasaha kwa walimu wenye changamoto za kimaadili. Pia tumekuwa tukitembelea shule zenye migogoro ili kuitatua mapema,” alisema Bw. Kilasi.

Kwa mujibu wa Bw. Kilasi, katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2026, walimu katika shule za msingi 193 na sekondari 51 wamefikwa na elimu ya kitaalamu kuhusu utumishi wao. Aidha, wakuu wa shule nao wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika

kusimamia nidhamu na kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Aliongeza kuwa pamoja na elimu hiyo, matumizi ya mifumo ya kidijitali kama TSCMIS yamerahisisha utoaji wa huduma kwa walimu, ikiwemo usajili na ufuatiliaji wa taarifa zao kwa ufanisi zaidi.

Katika kuimarisha ustawi wa walimu, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuboresha maslahi yao kupitia upandishaji wa vyeo, uthibitishaji kazini, pamoja na kuboresha mazingira ya kazi. Takwimu zinaonesha kuwa walimu 4,988 wamepandishwa vyeo, huku 277 wakithibitishwa kazini na 346 wakisajiliwa katika kipindi hicho.

Kwa upande wao, baadhi ya walimu wilayani humo wameipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa kuboresha sekta ya elimu, ikiwemo ujenzi wa miundombinu mipya ya shule, ajira za walimu wapya na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika ufundishaji.

Walisema hatua hizo zimechangia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani, kuongeza ufanisi wa ufundishaji na kujenga mazingira bora ya kujifunzia.

Aidha, walieleza kuwa mifumo ya kidijitali kama ESS na TSCMIS imerahisisha upatikanaji wa huduma za kiutumishi, kupunguza urasimu na kuongeza uwazi katika masuala ya ajira, uhamisho na tathmini ya utendaji kazi.

Kwa ujumla, utekelezaji wa miongozo, matumizi ya teknolojia na utoaji wa elimu kwa walimu umeendelea kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na ufanisi katika sekta ya elimu wilayani Njombe.



Bw. Msigala Philipo Kilasi katika picha ya kumbukumbu.



Afisa wa TSC Wilaya ya Njombe, Bi. Anasiana Mgani.



Afisa wa TSC Wilaya ya Njombe, Bw. Enost Mwakamele.

TSC LUDEWA YAWAFIKIA WALIMU 1,143, MASHAURI YA NIDHAMU YAPUNGUA KWA KIASI KIKUBWA

Na Mwandishi Wetu – Ludewa

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ludewa imewafikia walimu 1,143 kwa kuwapatia elimu na ushauri wa kitaalamu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma, hatua iliyochangia kupungua kwa mashauri ya nidhamu.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ludewa, Bw. Mathato Tematema, wakati wa mahojiano kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwahudumia walimu.

Alifafanua kuwa kati ya walimu hao, 709 ni wa shule za msingi na 388 wa sekondari, huku elimu hiyo ikitolewa kupitia ziara katika shule 140, zikiwemo shule za msingi 118 na sekondari 22.

Bw. Tematema alisema kuwa utoaji wa elimu hiyo kupitia ziara na machapisho mbalimbali umeongeza uelewa wa walimu kuhusu haki na wajibu wao, hali iliyosaidia kupunguza mashauri ya nidhamu kutoka 9 mwaka 2025 hadi shauri moja mwaka 2026.

“Lengo ni kuwawezesha walimu kuzingatia sheria na taratibu za kazi ili kuepuka makosa ya kinidhamu,” alisema.

Aliongeza kuwa matumizi ya miongozo ya utumishi yameendelea kuimarisha nidhamu na uwajibikaji kwa walimu kwa kuwapa mwongozo sahihi wa utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, alisema Serikali imeiwezesha TSC wilayani humo kwa vitendea kazi mbalimbali ikiwemo kompyuta, samani za ofisi na usafiri, hatua iliyorahisisha utoaji wa huduma kwa walimu.

Kwa upande wa mifumo ya kidijitali, Bw. Tematema alibainisha kuwa mfumo wa TSCMIS umerahisisha usajili wa walimu wapya na utunzaji wa taarifa za kiutumishi, ikiwemo mikataba ya ajira na uthibitisho kazini.

Kwa mujibu wa takwimu za wilaya hiyo, katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2026, walimu 1,560 wamepandishwa vyeo, walimu 200 wamethibitishwa kazini na walimu 274 wamesajiliwa na kuajiriwa.

Kwa ujumla, utoaji wa elimu ya utumishi kwa walimu umeendelea kuwa chachu ya kuimarisha nidhamu, kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji wa huduma za elimu wilayani Ludewa.



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ludewa, Bw. Mathato Tematema (katikati) akirwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Ludewa.



Maafisa wa TSC Wilaya ya Ludewa wakiwa safarini kwa boti kuelekea kutoa elimu kwa walimu.

WALIMU LUDEWA WATOA NENO

Na Mwandishi Wetu – Ludewa

Baadhi ya walimu wilayani Ludewa wameeleza kuridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha maslahi na mazingira ya kazi, wakibainisha kuwa zimeongeza ari na ufanisi katika utoaji wa elimu.

Mwalimu Faustin Komba wa Shule ya Msingi Kimbila alisema Serikali imefanya maboresho makubwa katika maslahi ya watumishi wa umma, ikiwemo nyongeza ya mishahara, upandishaji wa madaraja na uboreshaji wa miundo ya watumishi waliojiendeleza kielimu.

Kwa upande wake, Mwalimu Neema Magehema wa Shule ya Msingi Ludewa Mjini alieleza kuwa matumizi ya Mfumo wa Upimaji Utendaji Kazi (ESS) yamerahisisha

utekelezaji wa majukumu ya walimu, huku maboresho ya miundombinu ya shule yakichangia kuimarisha mazingira ya kujifunzia.

Naye Mwalimu Dora Ngwaya wa Shule ya Msingi Ludewa Kijijini alisema miongozo inayotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu imeimarisha maadili na nidhamu kwa walimu, huku akiishauri Serikali kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya TEHAMA na kutoa mafunzo zaidi kwa walimu ili kuendana na maendeleo ya teknolojia.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari Chief Kidulile, Mwl. Bara M. Kihanga, alisema matumizi ya mfumo wa TSCMIS yamerahisisha usimamizi wa taarifa za walimu na kuboresha utoaji wa huduma za kiutumishi, huku akibainisha kuwa maboresho ya mazingira ya kazi na ajira za walimu yameongeza motisha kazini.

TSC LUDEWA YAWAFIKIA WALIMU 1,143, MASHAURI YA NIDHAMU YAPUNGUA KWA KIASI KIKUBWA



Walimu wa Wilaya ya Ludewa wakipatiwa elimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi.



Baadhi ya walimu wilayani Ludewa wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa mafunzo.

SHULE YA CHIONA BAHY YANG'ARA KITAALUMA BAADA YA MABORESHO YA MIUNDOMBINU



*Mwalimu wa Shule ya Msingi Chiona,
Mwal. Amina Salumu Iddy.*

Na Mwandishi Wetu – Bahi

Shule ya Msingi na Awali Chiona, wilayani Bahi mkoani Dodoma, imeendelea kuonesha mafanikio ya kitaaluma baada ya kuboreshwa kwa mazingira ya kufundisha na kujifunzia, hatua iliyochangia kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi.

Kwa mujibu wa takwimu za shule hiyo, matokeo ya mtihamu wa darasa la saba yameimarika, ambapo mwaka 2024 shule ilishika nafasi ya pili kiwilaya, na mwaka 2025 ikashika nafasi ya kwanza kiwilaya na ya pili kimkoa.

Akizungumza katika mahojiano, Mkuu wa Shule hiyo, Bw. Godfrey Binamungu, alisema mafanikio hayo yanatokana na maboresho ya miundombinu yaliyotekelezwa kupitia Programu ya Kuboresha Uboresha Uboresha ya Awali na Msingi (BOOST), ambayo yameondoa msongamano wa wanafunzi darasani na kuboresha mazingira ya ujifunzaji.

“Awali tulikuwa na changamoto ya msongamano wa wanafunzi, hali iliyokuwa inaathiri utoaji wa elimu. Maboresho haya yameleta mazingira bora zaidi na kuongeza ufanisi wa ufundishaji,” alisema.

Alifafanua kuwa maboresho haya yamejumuisha ujenzi wa madarasa ya kutosha, miundombinu ya utawala, pamoja na huduma muhimu za shule, hali iliyowezesha walimu kufundisha katika mazingira tulivu na wanafunzi kujifunza kwa ufanisi zaidi.

Aliongeza kuwa kwa sasa shule ina wanafunzi 775 wa msingi, wanafunzi 100 wa awali na walimu 17, huku ongezeko la uandikishaji likichangiwa na ubora wa mazingira ya shule hiyo.

Kwa upande wake, Mwalimu Amina Salumu Iddy

alisema maboresho ya maslahi ya walimu na utatuzi wa changamoto za kiutumishi yameongeza ari ya kufundisha, jambo linalochangia moja kwa moja katika matokeo mazuri ya wanafunzi.

“Walimu wanapokuwa na utulivu na motisha, wanaweza kutoa elimu kwa ufanisi zaidi, na matokeo yake yanaonekana kwa wanafunzi,” alisema.

Aidha, walimu wa shule hiyo wameeleza kuwa uboreshaji wa mitaala na mazingira ya kujifunzia umechangia kuwaandaa wanafunzi kuwa na ujuzi na uwezo wa kujitegemea.

Kwa ujumla, mafanikio ya Shule ya Chiona yanaonesha umuhimu wa kuwekeza katika mazingira bora ya elimu kama njia ya kuongeza ufaulu wa wanafunzi na kuboresha ubora wa elimu nchini.



*Walimu wa Shule ya Msingi na Awali ya Chiona wakiwa
katika picha ya pamoja.*

UBORA WA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WAIMARIKA SHULE YA MSINGI CHEMBA B



*Mkuu wa Shule ya Msingi Chemba B,
Bw. Herman M. Kyssima.*



Darasa la awali katika Shule ya Msingi Chemba B.

Na Mwandishi Wetu – Chemba

Ubora wa ufundishaji na ujifunzaji katika Shule ya Msingi Chemba B, wilayani Chemba mkoani Dodoma, umeimarika kufuatia kuboreshwa kwa mazingira ya kazi kwa walimu na kujifunzia kwa wanafunzi.

Akizungumza katika mahojiano, Mkuu wa Shule hiyo, Bw. Herman M. Kyssima, alisema mabadiliko hayo yameongeza ufanisi darasani, ambapo walimu sasa wana uwezo mkubwa wa kuwafikia wanafunzi na kuwasaidia kujifunza kwa kina zaidi.

"Kwa sasa ufundishaji umekuwa rahisi zaidi na wanafunzi wanapata

muda na umakini unaostahili. Hii imeongeza uelewa wao darasani," alisema.

Aliongeza kuwa kupungua kwa msongamano darasani kumechangia kuboresha ushiriki wa wanafunzi wakati wa vipindi na kuongeza umakini wao katika masomo.

Kwa upande wa walimu, upatikanaji wa mazingira bora ya kazi umeongeza motisha na utulivu, hali inayochangia moja kwa moja katika ubora wa ufundishaji.

Mwalimu wa shule hiyo, Bi. Farida J. Kizanga, alisema maboresho ya huduma za kiutumishi na upatikanaji wa haki kwa wakati yameongeza ari ya walimu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

"Walimu wanapokuwa na uhakika wa maslahi yao na mazingira mazuri ya kazi, wanafanya kazi kwa moyo na matokeo yake yanaonekana kwa wanafunzi," alisema.

Aidha, uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia umechangia kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi, hususan katika ngazi ya awali, jambo linaloimarisha msingi wa elimu kwa watoto.

Kwa ujumla, uzoefu wa Shule ya Msingi Chemba B unaonesha kuwa kuboresha mazingira ya ufundishaji na kujifunzia kuna mchango mkubwa katika kuinua ubora wa elimu, kuongeza uelewa wa wanafunzi na kuimarisha utendaji wa walimu.



Nyumba ya walimu katika Shule ya Msingi Chemba B.



Jengo la darasa la awali pamoja na vifaa vya michezo.

UBORA WA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WAIMARIKA SHULE YA MSINGI CHEMBA B



Mwalimu wa shule hiyo, Bi. Farida J. Kizanga.



Walimu wa Shule ya Msingi Chemba B wakiwa katika picha ya pamoja.

MITAALA ITALETA MAGEUZI KATIKA SEKTA YA ELIMU NCHINI

Na mwandishi wetu-Bahi

Mkuu wa Shule ya Sekondari Bahi iliyopo Wilayani Bahi mkoai Dodoma Mwl. Sulusi Muganda Elienza alisema kuwa Mitaala mipya iliyoboreshwa italeta mageuzi katika sekta ya elimu nchini na hivyo kuchochea ari na moyo wakupenda kujifunza kwa nadharia na kwa vitendo kwa wanafunzi.

Ametoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa mahojiano na Afisa Uhusiano wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Tume ya Utumishi wa Walimu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwl. Elienza alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepania kuwaandaa wanafunzi wanaohitimu ngazi mbalimbali za elimu kuweza kujiandaa na soko la ajira pindi wanapo maliza masomo yao.

Alisema kuwa hatua hiyo inafuatia kuwa na mitaala hiyo inayowajengea stadi za maisha na soko la ajira, kwaasababu wanafundishwa kwa nadharia navitendo zaidi alisema.

Mwalimu Albert Mtuhi anayefundisha somo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuboresha Mitaala ili iendane na mahitaji ya sasa katika ulimwengu wa sayansi na Teknolojia.

Aliongeza kuwa wanafunzi watakapata ujuzi wa TEHAMA



Baadhi ya Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bahi wakiwa ndani ya Chumba cha Maabara wakiendelea na ujifunzaji wa vitendo

utawasidia kujajiri wenyewe katika masuala yote ya nayohusu Tehama ambayo ndiyo yapo kwa sasa katika shughuli za kila siku.

Naye Mwanafunzi, Abigael Moses aliishukuru Serikali kwa kuboresha mitaala na kuweza kujifunza kompyuta ambayo imewasaidia kupata habari na taarifa mbalimbali kupitia tovuti mbalimbali na matangazo ya nafasi za masomo na ufadhili wa nafasi za masomo na matangazo ya ajira.

Aidha, wanafunzi wanaosoma la kompyuta wamemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maboresho ya mitaala ambayo inawawezesha kujifunza kwa nadharia na kwa vitendo kitu ambacho kinawasaidia kuwapa ujuzi stahiki.

Aidha, Mwalimu Grace Rashid

Methusela aliishukuru Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kutoa miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku ambayo imewasaidia kuingia katika makosa na mashauri ya nidhamu kitu kinachoweza kuchafua taswira ya utumishi wa Mwalimu na hatimaye kuwapelekea kufukuzwa kazi.

Alisema kuwa katika kuhakikisha wanafunzi wanasoma masomo ya sayansi na kupata wataalamu mbalimbali Serikali ilitoa fedha kiasi cha shilingi za kitanzania milioni 30 kukamilisha jengo maabara ambalo linatumika kufanya mazoezi kwa vitendo jambo ambalo limewavutia wanafunzi kupenda masomo ya sayansi na kuamsha ari ya kujifunza zaidi.



Baadhi ya Wanafunzi wanaosoma masomo ya Kumpyuta katika shule ya Sekondari Bahi



Jengo la Maabara likiwa na baadhi ya vifaa vya Maabara katika Shule ya sekondari Bahi

TSC KONGWA YAWAFIKIA WALIMU, MASHAURI YA NIDHAMU YAPUNGUA

Na Mwandishi Wetu – Kongwa

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kongwa imewafikia walimu 406 kwa kuwapatia elimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma, hatua iliyochangia kupungua kwa mashauri ya kinidhamu.

Akizungumza katika mahojiano, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kongwa, Mwl. Edward Wilson Chamwela, alisema mashauri ya kinidhamu yamepungua kutoka 18 katika mwaka wa fedha 2021/22 hadi kufikia 7 mwaka 2025/26.

Alifafanua kuwa mafanikio hayo yanatokana na utoaji wa elimu ya mara kwa mara kwa walimu, matumizi ya miongozo ya utumishi pamoja na semina elekezi kwa waajiriwa wapya, hatua ambazo zimeongeza uelewa wa walimu kuhusu haki, wajibu na mipaka ya kazi zao.

"Lengo la mafunzo haya ni kuwawezesha walimu kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria na taratibu, na hivyo kuepuka makosa ya kinidhamu," alisema Mwl. Chamwela.

Aliongeza kuwa kupitia programu hizo, walimu wamepata uelewa mpana kuhusu masuala ya kiutumishi ikiwemo upandishaji vyeo, malipo ya stahiki kama fedha za likizo, maadili ya kazi, pamoja na taratibu za kushughulikia changamoto na malalamiko kupitia mamlaka husika.

Kwa upande wao, walimu wilayani

humu wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuboresha maslahi yao na mazingira ya kazi, hatua zilizoongeza ari na uwajibikaji kazini.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mnyakongo, Mwl. Safari Felix Kambadu, alisema maboresho ya maslahi ya walimu yameondoa changamoto za muda mrefu na kuongeza utulivu katika utekelezaji wa majukumu yao.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mnyakongo, Mwl. Safari F. Kambadu.

Naye Mwalimu Anna Shayo Alphonce alisema Serikali imeboresha utaratibu wa upandishaji vyeo kwa kuhakikisha walimu wanaostahili wanapanda kwa wakati na kupata stahiki zao kwa wakati, jambo lililoongeza morali wa kazi.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Mnyakongo, Mwl. Anna Shayo Alphonce.

Kwa upande wake, Mwalimu Bakari Mangi alieleza kuwa hatua hizo zimeimarisha nidhamu na kuwahamasisha walimu kufanya kazi kwa bidii zaidi.



Mwalimu Bakari Mangi.

Aidha, walimu hao wameipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya shule, kuajiri walimu wapya, pamoja na kuendeleza mitaala inayolenga kukuza ujuzi kwa wanafunzi, hatua zinazochangia kuboresha sekta ya elimu kwa ujumla.

Kwa ujumla, utoaji wa elimu ya utumishi kwa walimu umeendelea kuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha nidhamu, kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji wa huduma za elimu wilayani Kongwa.



Walimu wa Shule ya Msingi Mnyakongo wakiwa pamoja na Afisa TSC, Bw. Oscar Mpechi (katikati).



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kongwa, Mwl. Edward Wilson Chamwela.

TSC WANGING'OMBE YAWAFIKIA WALIMU 1,030, MASHAURI YA NIDHAMU YAPUNGUA

Na Mwandishi Wetu – Wanging'ombe

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Wanging'ombe imewafikia walimu 1,030 kwa kuwapatia elimu na ushauri wa kitaalamu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma, hatua iliyochangia kuimarika kwa nidhamu na kupungua kwa mashauri ya kinidhamu.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Wanging'ombe, Bi. Rukia Mwelelwa, wakati wa mahojiano kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwatumikia walimu.

Alifafanua kuwa kati ya walimu hao, 842 ni wa shule za msingi na 188 ni wa sekondari, huku elimu hiyo ikitolewa kupitia ziara katika shule 140, zikiwemo shule za msingi 126 na sekondari 14.

Bi. Mwelelwa alisema kuwa utoaji wa elimu hiyo, pamoja na usambazaji wa miongozo na vipeperushi, umeongeza uelewa wa walimu kuhusu haki na wajibu wao, hali iliyochangia kupungua kwa mashauri ya kinidhamu kutoka 26 mwaka 2021 hadi 7 mwaka 2026.

"Tunatoa elimu kwa njia mbalimbali ikiwemo ziara shuleni, semina elekezi na kupitia viongozi wa shule, lengo likiwa ni kuwawezesha walimu kuzingatia taratibu za kazi na kuepuka makosa ya kinidhamu," alisema.

Aliongeza kuwa TSC pia imewajengea uwezo wakuu wa shule 134 kuhusu wajibu wao kama mamlaka ya nidhamu, hatua iliyosaidia kuimarisha usimamizi wa walimu katika vituo vya kazi na kupunguza changamoto za uoto na ukiukwaji wa maadili.

Kwa upande wa maslahi, Bi. Mwelelwa alisema Serikali imeendelea kuboresha hali ya walimu kwa kuwapatia upandishaji wa vyao, ambapo walimu wa shule za msingi 661 na sekondari 417 wamepandishwa madaraja katika kipindi hicho.

Aidha, matumizi ya mifumo ya kidijitali kama TSCMS yamerahisisha utoaji wa huduma kwa walimu, ikiwemo usajili, upatikanaji wa mikataba na ufuatiliaji wa taarifa za kiutumishi kwa ufanisi zaidi.

Kwa upande wao, walimu wilayani humo wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuboresha maslahi yao, hususan katika upandishaji wa madaraja na ulipaji wa stahiki kwa wakati, hali iliyoongeza ari na utulivu kazini.

Walisema hatua hiyo imeondoa changamoto za muda mrefu za kucheleweshwa kwa madaraja na kuwarejeshea imani katika mfumo wa utumishi wa umma.

Aidha, walimu hao wameipongeza TSC kwa kuendelea kutoa miongozo mbalimbali ya utumishi, ikiwemo inayohusu maadili, nidhamu, ajira na maendeleo ya walimu, ambayo imewasaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Kwa ujumla, walimu na viongozi wa shule wameeleza kuwa utoaji wa elimu ya utumishi, matumizi ya mifumo ya kidijitali na uboreshaji wa maslahi umechangia kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na ubora wa elimu wilayani Wanging'ombe.



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Wanging'ombe, Bi. Rukia Mwelelwa, akizungumza wakati wa mahojiano ofisini kwake.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu